Zawadi

Yohana 3:16

Andiko limenakiliwa kutoka kwenye Biblia ya New King James Version®. Hatimiliki © 1982 by Thomas Nelson. Imetumiwa kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

Kambi ya Uwezo wa Mtoto: Kipawa

Yaliyomo yamesahihishwa 2014

Mifano imerudiwa upya 2018

Hati miliki © Huduma za L.I.T. 2016

Kimepigwa chapa na
Huduma ya L.I.T.
412 Mercedes, Suite F.
Fort Worth, TX 76126
www.leadersintraining.com

Kimeandaliwa na Clint May

Kimesahishwa na McMullin
Kimetafsiriwa na kupitiwa na Paul Mamba

Mifano imeingizwa na Katherine Holmes

Haki zote zimehifadhiwa. Hata sehemu moja ya kitabu hiki hairuhusiwi kunakiliwa bila kibali kili-chotolewa kwa maandishi kutoka kwenye Huduma ya L.I.T.

Kimetolewa na Mzungu Mpina Dar es salaam.

YALIYOMO

Utangulizi 5

Siku ya kwanza: "Uumbaji na anguko la mwanadamu".....7

Siku ya Pili: "Kuzaliwa kwa Yesu" 19

Siku ya Tatu: "Maisha ya Yesu na Miujiza".....31

Siku ya NNe: "Kifo cha Yesu na Kufufuka".....45

Siku ya Tano: "Paul: Maisha ya Mkristo" 59

Mafunzo ya Zawadi ya Biblia yametolewa
Kwa Kumbukumbu zenye upendoin za Claire Copeland,
Kwa upendo wake na mzigo wa kushirikisha Injili
Na kwa maombi mengi na msaada wa Huduma za L.I.T.

UTANGULIZI

Zawadi Kimeandikwa kwa ajili ya watoto wawafundishe watoto. Kila mtu anafurahia kupokea zawadi wakati wa Kristmas au wakati wa kumbukumbu ya kuzaliwa. Mungu anampa kila mtu zawadi ya Uzima wa Milele. Hiki kitabu ni maelezo ya msingi ya simulizi la zawadi ya Uzima wa milele ambayo Mungu hutoa kwa wanadamu wote. Simulizi la Upendo wa Mungu na utimilifu wa ahadi ya zawadi iliyotufikia kwa kupitia kwa Yesu Kristo na kujitoa kwake msalabani kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Mtu yeyote anaweza kuipokea zawadi hii katika kuliweka tumaini lake ndani ya Yesu Kristo, Akiamini kuwa alikufa kwa ajili ya dhambi zao na ya kuwa alifufuka kutoka kwa wafu.

Utangulizi

Kila somo linaanza na kifungo cha wazi kinachotoa taswira ya kitakachofundishwa siku hiyo. Linaweza pia kutoa taarifa za nyuma ili kusaidia kuelewa tafsiri ya simulizi la Biblia. Utangulizi pia unaweza kuonyesha kazi za vitendo zilizomo ndani ya somo.

Mpango wa kufundisha Mstari wa kukariri

Kila siku inao mstari maalum wa kukariri unaofundishwa kwa watoto kipindi cha somo la Biblia katika kundi. Mwanzo wa kila somo la siku, Mstari wa siku unaandikwa kwa maandishi makubwa ili watoto waweze kuona. Pia unaandikwa chini ya Mpango wa kufundisha Mstari wa kukariri uliopo kwenye ukurasa wa kwanza wa somo. Inakuwepo pia misemo iliyowekewa alama inayoelezea maana ya mstari husika. Anza kwanza na mstari wa kukariri kisha endelea na simulizi la siku. Simulizi litaleta maana pana kwenye mstari wa kukariri kwa kadri simulizi linavyoelezewa.

Vipengele vya Somo la Biblia

Kila somo la siku limebeba mpangilio wa vipengele vya somo vinavyoundwa na vipande vingi ambapo kila kimoja kinatoa mstari wa andiko, Maeneo muhimu ya kusisitiza katika simulizi la siku, na picha zinazowakilisha simulizi.

- **Kifungu cha Biblia** —Mwanzoni mwa kila Kipengele cha mpangilio wa somo la Biblia, utakikuta kifungu cha Biblia ambako simulizi limetolewa. Tenga mda kuweka alama kwenye Biblia yako na kuiweka tayari kwa kuwasomea wakati wa kipindi cha mafunzo katika kundi. Mara zote inakuwa vema kusoma kifungu moja kwa moja kutoka kwenye Biblia ili watoto watambue kuwa kweli unasoma kutoka Neno la Mungu.
- **Pointi Kuu**—Katika mfumo wa msemo, Vipengele vya somo la Biblia vinatoa pointi muhimu utakazosisitiza utakapokuwa unasimulia simulizi la Biblia la siku. Baadhi ya sehemu za simulizi zinanakiliwa moja kwa moja kutokana na maandiko ili kulinda uhalisia wa Neno la Mungu na kuepuka kuliondoa simulizi nje ya tafsiri ya Biblia. Hivi vipengele vinawekwa kwa lengo la kumsaidia mwalimu kwa kadri wanaipitia simulizi pamoja na watoto wanaowafundisha.
- **Picha**—Kwa upande wa pili wa kila ukurasa wa kila muhtasari wa somo la Biblia ipo picha inayoendana na simulizi. Unaweza kukikunja kitabu ili picha iwageukie watoto wakati simulizi linamuelekea mwalimu.

Kukata shauri na Mwaliko

Mwishoni mwa kila somo la siku, utakutana na maelezo mepesi na mchoro kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kuelewa kuwa dhambi inatutenga na Mungu. Hili linafuatiwa na maelekezo maalum juu ya jinsi ya kumwongoza mtoto alimo kundini kwenye maamuzi binafsi ya kumfuata Yesu Kristo.

“Kwa maana wote wametenda dhambi na kupun-gukiwa na utukufu wa Mungu.”

(Warumi 3:23)

SIKU YA KWANZA
"UUMBAJI NA ANGUKO LA MWANADAMU"

Utangulizi

Somo la Letu la leo linahusiana na Uuumbaji wa Dunia na kiumbe mojawapo cha ajabu kuliko vyote —Mtu. Kwa nini mtu ni wa kipekee? Tumeu,bwa kwa mfano wa Mungu. Mungu amesema, " Na TUMFANYE mtu kwa mfano wetu" (Mwanzo 1:26a). Mungu anamuona Mtu kama kiumbe wa ajabu katika uumbaji wote, Hivyo alimpa Mtu jukumu la la kutawala uumbaji wote. Kwa wakati huo, Mungu alimpa Adamu Amri na Eva amri ya kutii na kuiheshimu. Amri kuu katika Bustani ya Edeni ilikuwa, " Lakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya msile, maana siku mtakayokula hakika mtakufa" (Mwanzo 2:17). Aliwaonya kuwa siku watakapo kula watakufa hakika.

Mtu anaweza kujiuliza dhambi zilitokana na nini, na zilianzia wapi. Zote zilianzia katika Bustani. Kutokana na kosa moja kubwa, Dhambi ziliingia ulimwenguni mwote. Utukufu wa simulizi la uumbaji ni kwamba japokuwa Adamu na Eva walikosea sana, Mungu aliahidi kumleta Mkombozi siku moja. Mungu ni Mtakatifu na Mkamilifu, na anatarajia kuona wanadamu wote wakiwa watiifu kwa mari zake na mamlaka na Neno lake. Adamu na Eva hawakutii, hivyo walipoteza kila kitu chema walichopewa na Mungu.

Mpango wa Kufundisha kifungu cha Kukariri

Kifungu cha kukariri
" Kwa maana **wote watenda** Dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."(Warumi 3:23)

Ufafanuzi wa Kifungu cha Kukariri
- Biblia isemapo " Wote" inamaanisha kila mtu.
- Je umewahi kulenga shabaha? Unatarajia nini haswa unapokuwa unailenga shabaha? (Mtoto wa jicho) Kwa ajili ya Dhambi, Umemkosa Mungu moja kwa moja. Hata hujaweza kuikaribia shabaha.
- Dhambi ni jambo lolote unalofikiri, unalosema, unalotenda au usilotenda lisilompendeza Mungu.
- Hebu tuutaje mstari kwa pamoja: Kwa kuwa wote wametenda Dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." (Warumi 3:23)

SIKU YA KWANZA

Muhtasari wa Somo la Biblia

Uumbaji

Mwanzo 1:1-31

- Biblia inasema katika Mwanzo 1:1, **"Hapo Mwanzo Mungu aliziumba Mbingu na Nchi."** Mungu aliumba kila kitu ndani ya siku sita.

- **Mungu aliumba** Mchana na Usiku, Mbingu na Bahari,Nchi na Mimea, Jua, Mwezi na Nyota, Ndege na viumbe wa Baharini, na wanyama.

- Siku ya sita Mungu aliumba kiumbe wa maalum na wa kipekee katika viumbe vyote—Wewe na Mimi! **Mungu alimuumba Mtu kwa mfano wake, na Mungu akamuweka Mtu kuwa mwangalizi wa uumbaji wote.** Mungu aliwaumba Mwanamume na Mwanamke.

Mungu alikiumba kiumbe kamili, lakini jambo Fulani lilitokea na likaharibu mambo.

SIKU YA KWANZA

Anguko la Mwanadamu

Mwanzo 2:16-17; 3:1-5

- "Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustanini waweza kula," (Mwanzo 2:16)

- "'...Walakini matunda ya mti wa ujuzi waa mema na mabaya **usile**, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo **utakufa** hakika." (Mwanzo 2:17)

- "Basi **nyoka** alikuwa **mwerevu** (Mjanja) kuliko wanyama wote wa mwituni aliowafanya BWANA Mungu." (Mwanzo 3:1a) **Kazi: Tengeneza umbo la nyoka kwa mikono yako mwenyewe kasha tengeneza sauti nyembamba.**

- "Kisha akamwambia mwanamke, **'Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani"?'** Na Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustani twaweza kula." (Mwanzo 3:1b-2)

- "...Lakini matunda ya **mti ulio katikati ya bustani** Mungu amesema, **Msiyale** wala msiyaguse, msije mkafa." (Mwanzo 3:3)

- "Kisha nyoka akamwambia Mwanamke , **Hakika hamtakufa."** (Mwanzo 3:4)

- "Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi **mtakuwa kama Mungu**, mkijua mema na mabaya." (Mwanzo 3:5)

Dhambi ya Adamu na Eva Bustanini

Mwanzo 3:6-7

- "Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi **alitwaa katika matunda yake akala**." (Mwanzo 3:6a) **Kazi:** Jifanye kana kwamba umeshikilia mikononi mwako tunda lililokatazwa, limege , kisha mpe na jirani yako.

- "Akampa na mumewe, **naye akala**." (Mwanzo 3:6b)

- "Ndipo **Wakafumbuliwa macho wote wawili** wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo." (Mwanzo 3:7) **Uliza:** Kwa nini unadhani walishona majani ya Mtini?

- **Uliza: Unadhani Adamu na Eva walijibuje** walipomuona Mungu kwa mara ya kwanza. ?

Acha tuone Mungu alivyojibu matendo yao

Siku ya Kwanza

Dhambi ya Adamu na Eva bustanini—Madhara

Fanya vitendo: Chi ya watoto wachukue nafasi mbali mbali katika simulizi. Utahitaji watoto wacheze nafasi ya Mungu, Adamu, Eva na Nyoka.

Mwanzo 3:8-24

- Kisha " **Wakasikia sauti ya Bwana Mungu**, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; **Adamu na mkewe wakajificha**, kati ya miti ya bustanini, Bwana Mungu asi-waone." (Mwanzo 3:8)
- "**Bwana Mungu** akamwita Adamu, akamwambia, **Uko wapi?**" (Mwanzo 3:9)
- Akasema, "Nalisikia sauti yako bustanini, **nikaogopa** kwa kuwa mimi ni uchi; **ni-kajificha**." (Mwanzo 3:10)
- Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? **Je! Umekula wewe matunda ya mti** niliyokuagiza usiyale?" (Mwanzo 3:11)
- Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala**. (Mstari 12) Kazi:** Waelekee watoto kadhaa na fanya kana kwamba unawalaumu.
- Bwana Mungu akamwambia mwanamke, **Nini hili ulilolifanya?"** (Mstari 13a)
- **Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala.** (Mstari 13b) **Kazi:** Muelekezee ji-rani yako kidole kisha mwambie ni wewe ndiye uliyefanya!"
- **Bwana Mungu akamlaani nyoka** kwa kile alichotenda (Mstari 14)
- "Nami nitaweka **uadui [Vita na magombano] kati yako na huyo mwanamke**, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino." (Mstari 15)
- Laana dhidi ya shetani ni kwamba siku moja **Mkombozi atatokea** na kumponda kicha. Mkombozi ataiharibu mauti na kurejesha uhusiano uliovunjika kati ya mwanadamu na Mungu.
- **Mungu alimuhukumu Eva kwa kile alichotenda.** Alisemae Atakuwa na uchingu mwingi wakati wa kuzaa kwake. (Mstari 16)
- **Mungu alimpa malipizi Adamu kwa yale aliyoyatenda.** Alimwambia Adamu kuwa ata-takiwa kufanya kazi kwa nguvu maisha yake yoye ili kujipatia chakula. (Mstari 17-18)
- **Mungu aliwaondoa Adamu na Eva bustanini** ili kwamba wasije wakala katika tunda la mti wa Uzima na wakaishi milele. (Mstari 22-23)
- **Mungu aliweka Malaika kwenye lango la bustani** na upanga wa moto kuilinda njia iele-keayo kwenye Mti wa Uzima. (Mstari 24)


Kutengwa na Mungu
Mungu
Dhambi
kufanywa Haki na Mungu
Mungu
Yesu
Dhambi
Siku ya kwanza

Dhambi zilitutenga wewe na Mimi kutoka kwa Mungu (Nukuu Warumi 6:23)

Dhambi ni chochote unachokifikiri, Unachokisema, unachotenda, au usichotenda na hikimpemdezi Mungu.

Je unaweza kutaja baadhi ya Dhambi? (Kusema uongo, Kudokoa, Kuiba, Kuwachukia wengine, Kutowatii wazazi, Kumdharau muhitaji nk…)

Kwa sababu ya Dhambi zako, umetengwa na Mungu, na umepotea**. Kazi**: Elekeza sehemu yenye ufa kati ya wewe na Mungu kwenye picha iliyopo kushoto kwako.

Adhabu ya Dhambi za Adamu na Eva ilikuwa **Mauti**.

Itendee Kazi: Wachague watoto waigize juu mtengano kati ya Mungu na Mwanadamu. Utawahitaji watoto waigize nafasi ya Mungu, Yesu Kristo na Mtenda dhambi. .

Kumtenga “Mungu” na “Mwenyedhambi” mbali . Elezea kwamba dhambi zinatutenga sisi na Mungu na mbingu. Lakini alipokuja Yesu duniani kama zaidi ya miaka 2000 iliyopita, Alikuja kututengenezea njia kuelekea kwa Mungu. Mpate” Yesu” Enenda mbele na shika mkono wa “mwenye dhambi” na mwelekeze kwa “ Mungu”. (Kwa mkono wako, Ifunike picha yenye msalaba wa rangi ya udongo ili kuyaaelezea madhara ya dhambi na kile alichokifanya Yesu.)

Maamuzi

Illi kuipokea zawadi ya Mungu ya Uzima wa milele, **Ni lazima ABC:**

A—Admit = Kubali mbele za Mungu kuwa umetenda dhambi na umetenda mabaya. Kumbuka dhambi ni jambo lolote unalofikiri, usemalo, utendalo, au usilolitenda lisilompendeza Mungu.

B—Believe = Amini Kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako na alifufuka kutoka kwa wafu.

C—Choose = Chagua kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi, inamaana Unamfanya yeye kuwa kiongozi wa maisha yako.

Mwaliko wa kufanya chaguo

Tafadhali Inamisha vichwa vyenu na funga macho sasa.

Sasa naomba, au sema na Mungu. **Kazi:** Waombee watoto ili wawe na moyo wa kufanya maamuzi. Usimalize maombi maombi yako na “ **Amina”** kwanza.

Kama ungetamani kumwomba Yesu akuokoe kutokana na dhambi zako leo, tafadhali inua kidole chako sasa.

Iwapo umeinua kidole chako, simama sasa na ondoka elekea _____ (Elekeza eneo) mahali ambapo yupo mtu atakaye zungumza na wewe kuhusu jinsi ya kumfanya Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wakko.

Kazi: Baada ya kila mtoto kusimama na kuondoka, **malizia maombi yako** kwa kumshukuru Bwana kwa msamaha na maisha ya milele. Kisha malizia na “ **Amina**”

Siku ya kwanza: Maswali ya Rejea ya somo

1. Ni nani aliyeumba vitu vyote? (Mungu)
2. Biblia Inasema, “ Hapo mwanzo _____ aliziumba Mbingu na nchi.” (Mungu)
3. Ni kipi cha kipekee Mungu alichokiumba siku ya sita? (Alimuumba mtu kwa mfano wake.)
4. Ni mti gani Mungu alisema Adamu asile? (Mti wa ujuzi wa mema na mabaya)
5. Ni kipi shetani au nyoka, alichomwambia Eva kuhusu matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya? (**HAMTAKUFA** hakika.)
6. Tunaliitaje tukio la mtu kutokumtii Mungu? (Dhambi)
7. Je! Biblia Inasemaje kuhusu Dhambi? (Wote wametenda Dhambi. Wakumbushe, “Dhambi ni jambo lolote unalofikiria, unalolisema, unalolifanya, au usilolifanya lisilompendeza Mungu.”)
8. Ni ahadi gani Mungu alimpa Adamu na Eva? (Kwamba angemtuma Mkombozi.)
9. Je Adamu na Eva walikufa mara baada ya kula matunda ya mti? (Ndiyo kwa uhalisia)
10. Nani anaweza kututajia mstari wa kumbukumbu wa leo? (Warumi 3:23, “ Kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.”)

Siku ya Kwanza: Bangili za Kubuni



<u>Vifaa hutolewa</u>:
Kamba ya ngozi na Shanga katika rangi zifuatazo: Nyeusi, Nyekundu, Nyeupe, Manjano, na Kijani. (Kila mtoto atatakiwa kuwa na kamba na kila aina ya rangi ya shanga). Kamba zinaweza kupatikana kwenye stationary. Tafsiri ya kila rangi ya shanga itaandikwa kwenye kipande cha karatasi atakachopewa kila mtoto.

<u>Jinsi ya kuitengeneza</u>:

1. Kata kipande cha ngozi chenye urefu wa Nchi 8—10.
2. TFunga fundo kwenye urefu wa takriban nchi tatu kutoka ncha moja ya kamba hiyo..
3. Chomeka shanga kwenye hiyo kamba kwa mtiririko wa Rangi kama ifuatavyo: Kijani, Manjano, Nyeupe na Nyekundu, na Nyeusi.
4. Baada ya kuchomeka shanga zote, unga ncha zote mbili kwa kuanzia pale zinapoishia shanga.

<u>Ujumbe:</u> (Mpe kila mtoto kipande cha karatasi kikiwa na tafsiri ya kila rangi ya shanga juu yake.)

Hiyo bangili ni njia kubwa ya kuelewa Ujumbe wa Injili.

- **Nyeusi: Anza na giza Shanga** (Nyeusi). Biblia inasema, “ Kwa maana mshahara wa dham,bi ni **mauti**, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.” (Warumi 6:23). Kumbuka, Kupitia dhambi ya Adamu na Eva bustanini, Dhambi iliingia ulimwenguni kasha mauti yakatokea kama adhabu ya dhambi.
- **Nyekundu:** Shanga Nyekundu inasimama mahali pa **damu** ya Yesu Kristo na kifo chake msalabani kwa ajili ya msamaha wa dhambi. 1Wakorintho 15:3-4 inasema, “ Kwa maana naliwatolea hapo kwanza yale niliyoyapokea mwenyewe: kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo maandiko, na kuwa alizikwa, na kuwa alifufuka siku ya tatu kama yanenavyo maandiko.” Mungu alimtuma Yesu miaka mingi baada ya uumbaji ili kuibeba adhabu ya dhambi zetu.
- **Nyeupe:** Iwapo unaamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako na kuwa alifufuka siku ya tatu, utakuwa na uzima wa milele. Utafanyika **Mwana wa Mungu**. Yohana 1:12 inasema, “Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndiyo wale waliaminio jina lake.”
- **Manjano:** Shanga ya Manjano inasimama nafasi ya **Mbingu.** Unapofanyika Mwana wa Mungu, unapokea ahadi ya uzima wa milele mbinguni pamoja na Mungu. Ufunuo 21:21 Inaelezea Mbingu: “Mitaa ya mji ule ilikuwa Dhahabu tupu.”
- **Kijani:** Mara unapompokea Yesu kama Mwokozi na Bwana wako, Utahitaji **kukulia** imani yako kwa kuitumia Biblia kama kiongozi chako. 2Petro 3:18a Inasema, “Bali zidi kukua katika neema na kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo.”

“Kwa Maana jinsi hii Mungu aliupenda Ulimwengu, Hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa Milele.”

(Yohana 3:16)

Siku ya Pili
"Kuzaliwa kwa Yesu"

Utangulizi

Wakati ulipowadia. Mwokozi aliyeahidiwa alikuwepo hapa kwa maelfu ya miaka, waisrael walimsubiri masiya, ambaye angewakomboa kutokana na utumwa wao. Ni kwa sehemu ndogo walitambua kuwa mpango wa Mungu ni tofauti sana na walivyodhani. Mungu alimtuma mwanawe pekee, " Zawadi" kwake aliyepotea na na kwa ulimwengu unaokufa ili kutukomboa kutokana na dhambi zetu.

Yesu aliziacha mbingu, sehemu ya heshima na raha kamili, aliuacha utukufu wa nyumbani kwake na kuja duniani. Akazaliwa kwenye hori la ng'ombe, na kitanda chake kilikuwa malishio ya ng'ombe. Alikuja kwa lengo la kurejesha mahusiano kamili ya mwanadamu yaliyoharibika kati yake na Mungu Baba. Yesu ndiye uwakilishi wa kipawa cha uzima wa milele tulichostahili kupokea katika kuiweka imani na tumaini letu kwake atuokoe.

Mpango wa kufundisha kifungu cha kukariri

Kifungu cha kukariri

"kwa maana jinsi hii **Mungu aliupenda ulimwengu**, hata akamtoa mwanawe pekee ili **kila mtu amwaminiye** asipotee bali awe na **uzima wa milele**. " (Yohana 3:16)

Maelezo ya Kifungu cha kukariri

- Kwa ajili ya dhambi, ulimwengu (Yeyote aishie Duniani) amewekewa kufa (Kupotea).
- Mungu aliupenda sana ulimwengu kuliko yeyote awezavyo kufikiria.
- Alimtuma mwanawe Yesu Kristo kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.
- Yeyote anayeamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu na kuwa alikufa kwa ajili ya dhambi zake, atapokea Uzima wa Milele.

Muhtasari wa Somo la Biblia

Malaika Anazungumza na Mariamu

Kumbuka, jana tulizungumzia anguko la mwanadamu kwa sababu ya dhambi. Kwa sababu ya Adamu na Eva, Dhambi iliingia ulimwenguni mwote, na wote tumekuwa wenye dhambi kama matokeo ya chaguo lao mbaya. Mungu aliweka ahadi kwa Adamu na Eva kutenda dhambi kwamba angemtuma Mkombozi. Leo tutazungumzia juu ya ahadi ya Mungu kumleta Mkombozi.

Luka 1:30-32a; 1:35; 2:4-7

- "Kisha malaika akamwambia, Usiogope Mariamu, kwa kuwa umejaliwa neema na Mungu, **tazama utachukua mimba**, nawe utamzaa Mwana, na we utamwita jina lake Yesu. Atakuwa Mkuu, Nawe utamwita Mwana wa aliye juu.'" (Luka 1:30-32a)

- "Naye Malaika akamjibu akisema, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na **uweza wake aliye juu utakufunika**; kwa sababu hiyo, pia, Mtakatifu atakayezaliwa ataitwa Mwana wa Mungu.'" (Mstari. 1:35)

- Baadae **Yusufu alipogundua kuwa Mariamu ana mimba** na mtoto tumboni mwake, alidhamiria kumwacha.

- **Malaika akamtokea Yusufu kwenye ndoto na kumwambia asimwache mkewe Mariamu** maana alimbeba Mwana wa Mungu.

- **Yusufu akamuoa Mariamu kuwa mke wake wa ndoa**.

Kitoto Yesu kilikuwa tumboni mwa Mariamu
hadi wakati wa kuzaliwa ulipowadia.

Siku ya Pili

Kuzaliwa kwa Yesu

Luka 2:4-7

- "**Yusufu alipanda kutoka Galilaya,** Nje ya mji wa Nazareti, Katika Uyahudi, **Mjini mwa Daudi ulioitwa Betelehemu,** maana alikuwa wa mbari na ukoo wa Daudi." (Mstari. 4)

- Akaenda kujiandikisha pamoja na **Mariamu**, Mke wake aliyemposa. **Aliyembeba Mtoto**." (Mstari. 5)

- "Ikatokea, walipokuwepo hapo, **siku zake za kuzaa zilitimia**." (Mstari. 6) **Kazi:** Onyesha sehemu ya uso wa Mtoto kwenye picha.

- "Akamzaa mtoto **wake wa kiume kifungua tumbo**." And she brought forth **her firstborn Son**." (v. 7a)

- "...Na akamkunja katika mavazi ya kitoto, na **akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe**." (Mstari. 7b)

- "
- Kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni." (Mstari 7c)

- Yusufu na Mariamu **waliuona uwepo wa Mungu**. Walipoutazama uso wa Yesu, Walikuwa wakiutazama uso wa Mungu. **Yesu ni Mungu**!

Yusufu na Mariamu siyo pekee waliofahamu kuhusu kipawa hiki cha kipekee.

Siku ya Pili

Kifo cha Yesu Kilitaarifiwa

Luka 2:8-15

- Walikuwepo walinzi makondeni **karibu na Bethlehemu.** (Mstari 8)
- **Malaika wa Bwana akawatokea**, na **Utukufu wa Bwana ukawaangazia pande zote**." (Mstari. 9)
- Malaika akawaambia, **"Msiogope, kwa kuwa nawaleta habari njema ya furaha kubwa."** (Mstari 10)
- "Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, **Mwokozi,, ndiye Kristo**." (Mstari 11)
- Malaika aliwaambia kuwa **wangemkuta mtoto ameviringishwa katika mavazi ya kitoto na kulazwa katika hori la kulia Ng'ombe**. (Mstari 12)
- Kwa wakati huo, **Idadi kubwa ya malaika** walisimama mbele yao na **kuanza kuimba**. (Mstari 13)
- "**Atukuzwe Mungu juu mbinguni**, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia!" (Mstari 14)
- Baada ya malaika kuondoka, Wachungaji walitaka **kwenda na kumuona mtoto aliyezaliwa katika Bethlehem**. (Mstari 15)

Wachungaji walienda Bethlehem
kumuona Yesu, Mwokozi.


Kutengwa na Mungu
Mungu
Dhambi
kufanywa Haki na Mungu
Mungu
Yesu
Dhambi
Siku ya pili

Kwa nini Yesu alikuja Duniani?

Yesu alikuja Duniani kwa ajili ya **dhambi zetu**.

Mungu kwa kina anatupenda sana, Na **anataka sisi tuwe na Uzima wa milele.** Kwa ajili ya dhambi zetu, tumetengwa na Mungu. (Elekeza kwenye picha upande wa kushoto).

Vitendo: Chagua watoto watatu wacheze kwa vitendo juu ya utengano kati ya Mungu na Mwanadamu. Unahitaji watoto wacheze nafasi ya Mungu, Yesu na mwanadamu aliyepotea.
Mtenganishe "Mungu" na "Mwanadamu aliyepotea" kwa mbali kabisa. Elezea kwamba dhambi ndizo zinatutenganisha na "Mungu" na Mbingu. Bali alipokuja Yesu duniani zaidi ya miaka 2000 iliyopita, Alikuja kuandaa njia ielekeayo kwa Mungu. Mruhusu "Yesu" atawale na Ashike mkona wa "mwanadamu aliyepotea" na kumuelekeza kwa "Mungu."

Dhambi inatutenga wewe na mimi kwa Mungu.

Warumi 6:23 Katika Biblia inasema, "Kwa kuwa **mshahara wa dhambi** ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa Milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."

Dhambi ni jambo lolote unalolifikiri, usemalo, utendalo, au kutotenda lisilimpendeza Mungu.

Je unaweza kutaja baadhi ya dhambi? (Uongo, Kuiba, Kudokoa, kuwaumiza wengine, , kutowaheshimu wazazi, Kutokumjali muhitaji, nk…)

Kwa ajili ya dhambi zako umetengwa na Mungu, na umepotea. **Kazi:** Elekeza kwenye Ufa kati ya Mungu na Mwanadamu.

Kwa wote wametenda dhambi, Mungu aliitimiza ahadi yake na **akamtuma Mwokozi atuokoe kutokana na dhambi**. **YEsu hakutenda dhambi kamwe. Alikuwa mkamilifu.**

Maamuzi

Illi kuipokea zawadi ya Mungu ya Uzima wa milele, **Ni lazima ABC:**

A—Admit = Kubali mbele za Mungu kuwa umetenda dhambi na umetenda mabaya. Kumbuka dhambi ni jambo lolote unalofikiri, usemalo, utendalo, au usilolitenda lisilompendeza Mungu.

B—Believe = Amini Kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako na alifufuka kutoka kwa wafu.

C—Choose = Chagua kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi, inamaana Unamfanya yeye kuwa kiongozi wa maisha yako.

Mwaliko wa kufanya chaguo

Tafadhali **Inamisha vichwa vyenu** na funga macho sasa.

Sasa naomba, **au sema na Mungu**. **Kazi:** Waombee watoto ili wawe na moyo wa kufanya maamuzi. Usimalize maombi maombi yako na " Amina" kwanza.

Kama ungetamani kumwomba Yesu **akuokoe kutokana na dhambi zako** leo, tafadhali inua kidole chako sasa.

Iwapo umeinua kidole chako, **simama sasa na ondoka elekea** _____ (Elekeza eneo) mahali ambapo yupo mtu atakaye zungumza na wewe kuhusu jinsi ya kumfanya Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wakko.

Kazi: Baada ya kila mtoto kusimama na kuondoka, **malizia maombi yako** kwa kumshukuru Bwana kwa msamaha na maisha ya milele. Kisha malizia na " Amina"

Siku ya Pili: Maswali ya Rejea ya Somo la Biblia

1. Je malaika alisemaje kuhusu jina la mtoto atakaye zaliwa na Mariamu? (Mwana wa Mungu)
2. Je! Yesu alizaliwa wapi? (Bethlehem katika hori la kulia Ng'ombe)
3. Ni lipi jina la Baba mlezi wa Yesu? (Yusufu)
4. Kwa nini Yesu alizaliwa Horini? (Haikuwepo nafasi katika vyumba vya kulala wageni.)
5. Ni nani aliyewaambia wachungaji kuhusiana na kuzaliwa kwa Yesu? (Malaika)
6. Nini kilitokea baada ya malaika kuwataarifu wachungaji kuhusu kuzaliwa kwa Yesu? (Kundi kubwa la maliaka lilikuwa linamsifu Mungu, na wachungaji walielekea Bethlehemu kumuona Yesu.)
7. Kwa nini Yesu alikuja duniani? (Alikuja kutuokoa dhidi ya dhambi.)
8. Je Yesu aliwahi kutenda dhambi? (Hapana, alikuwa mkamilifu.)
9. Dhambi ni nini? (Dhambi ni jambo lolote unalolifikiria,utendalo au kutotenda lisilompendeza Mungu.)
10. How do we receive God's forgiveness for our sins? (We believe in Jesus, God's Son.)

Siku ya Pili: Umbo la picha ya mkono



Vitendeakazi:
Vijiti kadhaa vya rangi mbali mbali, pini za vishikizo, Gundi ya ndogo ya maji. Vifaa hivyo vinaweza kupakatika Stationary.

Jinsi ya kuitengeneza:
Unganisha ncha za vijiti vya rangi kwa kutumia gundi. Hakikisha eneo la kati linatosheleza andiko la siku. Andaa nakala za kutosha za Mstari wa siku kwa ajili ya kila mtoto (Angalia ukurasa unaofuata). Tumia pini za vishikizo kulipamba umbo.

Ujumbe:
Umbo hili la picha ni kumbukumbu ya upendo wa Mungu alionao kwa kila mmoja wetu. Kumbuka Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu ili tupate msamaha wa dhambi zetu na kuupokea uzima wa milele katika kumwamini. Andiko hili linapatika kwenye Biblia, Neno la Mungui, na ni ahadi ya upendo wa Mungu kwako.

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanae wa pekee, ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele.”

Yohana 3:16

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanae wa pekee, ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele.”

Yohana 3:16

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanae wa pekee, ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele.”

Yohana 3:16

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanae wa pekee, ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele.”

Yohana 3:16

“Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika kristo Yesu Bwana wetu.”

(Warumi 6:23)

Siku ya tatu
"MAISHA YA YESU NA MIUJIZA"

Utangulizi

Yesu alizaliwa kutokana na mwanamke, Mariamu, na alikuwa mwanadamu kamili. Alikuwa pia mwana wa Mungu na alikuwa Mungu kamili. Aliwapenda watu, na aliwaonyesha upendo wake kwa kuwafufua wafu, kuwaponya wagonjwa, kuwalisha wenye njaa, na kuwaokoa kutokana na dhambi. Ni Mungu pekee mwenye uwezo wa kutenda miujiza aliyoifanya Yesu. Alifanya kutokana na Upendo, lakini miujiza yake ulikuwa udhihirisho wa asili yake ya Uungu—Kwamba alikuwa Mungu aliyevaa mwili. Yesu alitaka watu waamini kuwa hakika Yeye ni Mwana wa Mungu ili kwa kuamini hivyo wapate uzima wa Milele.

Yesu alikuwa Mungu, na alifanya miujiza mingi kuthibitisha kuwa alikuwa na mamlaka juu ya kila kilichoumbwa.

Mpango wa Kufundisha Mstari wa kukariri

Mstari wa Kukariri

"Kwa maana **mshahara wa Dhambi ni mauti,** bali **karama ya Mungu ni uzima wa milele** katika Kristo Yesu Bwana wetu." (Warumi 6:23)

Maelezo ya mstari wa kukariri

- Neno "Mshahara" linamaanisha tuzo mtu analostahili kulipwa.
- Dhambi zina malipo yake au gharama.
- Dhambi ni jambo lolote unalolifikiria,utendalo au kutotenda lisilompendeza Mungu.
- Tunastahili kifo, bali karama ya Mungu ni uzima wa Milele kupitia Yesu Kristo.

Siku ya tatu

Muhtasari wa somo la Biblia

Yesu amfufua Binti

Vitendo: Teua watoto wane wasaidie kuigiza sehemu ya mama, baba, Yesu na binti wa Yairo.
Binti na alale chini, wazazi wafunike nyuso zao kama ishara ya kuonyesha uchungu na kulia. Soma sehemu ya simulizi iliyosalia, kwa waruhusu watoto waigize kwa kadri unavyoendelea kusimulia.

Marko 5:21-24a, 35-43

- **Yesu** alikuwa akisafiri na **kuvuka bahari ya Galilaya.**
- **Yairo,** kiongozi wa sinagogi [kanisa], alimjia yeye **na kumuomba** aje nyumbani kwake na **kumponya binti yake.** (Mstari 22-23)
- Baaddhi **ya watu kutoka nyumbani kwa Yairo walimjia**. (Mstari 35a)
- "'**Binti yako amekufa tayari**. Kwa nini Umsumbue tena Mwalimu?'" (Mstari 35b)
- Yesu hakuwasikiliza na akamwambia Yairo, **" Usiogope; wewe amini tu."** (v. 36)
- Walipofika nyumbani kwa Yairo, **watu walikuwa wanalia** kwa sababu **binti amekufa.** (Mstari 38)
- Yesu aliingia ndani ya nyumba na kuwaambia watu, **" mtoto hajafa,** bali amelala." (Mstari 39)
- **Walimcheka Yesu.** (Mstari. 40a) **Kazi:** Mruhusu kila mmoja acheke kwa sauti kubwa na aseme, "Amekufa!"
- Akiwa na wazazi pamoja na wanafunzi wake, **Yesu aliingia hadi alipokuwa amelazwa Yule binti** (Mstari 40)
- Yesu alimshika binti mkono na akamwambia, **" Binti, nakuambia, amka!"** (Mstari 41)
- Mara tu Yesu alipotamka maneno hayo, **Binti aliinuka na kutembea."** (Mstari 42a)
- **Watu walishtuka na kushangazwa** na muujiza wa Yesu. **Kazi:** Waamuru kila mmoja afunike uso kwa mikono yake na kuigiza kama vile wamepatwa na mshangao kwa kile walichokiona.

Kimuujiza Yesu amerejesha uhai wa binti;
Pia alimponya kipofu.

Nifuatisheni mimi: "Mungu pekee ndiye atendaye miujiza."
"Jesus is God!"

Siku ya tatu

Yesu amponya kipofu

Marko 8:22-25

- **Yesu alienda katika mji wa Betesaida.** (Mstari. 22a)
- Watu Fulani **"walimleta mtu kipofu kwa Yesu,** kasha **wakamuomba amguse."** (Mstari 22b)
- **Walitamani Yesu amponye Yule kipofu.**
- **Yesu akamungoza Yule kipofu nje ya kijiji** kwa kumshika mkono**.** (Mstari 23a)
- Yesu **akamtemea mate machoni pake** kasha **akamuwekea mikono.** (Mstari 23b)
- Yesu alimuuliza kama anawezaa **kuona kitu**. (Mstari 23c)
- Yule mtu akasema **anaona watu,** lakini **walikuwa kama miti.** (Mstari 24)
- Yesu akamgusa tena, **na akawa mzima. Sasa aliweza kuona.** (Mstari 25b) **Kazi:** Waamuru watoto wafunge macho kwa kuyakaza na kuyafunika kwa mda. Kasha waambie waondoe mikono na kufumbua macho yao. Wafafanulie kuwa mtu huyu alikuwa gizani na asingeweza kuona chochote. Yesu alimponya mtu Yule, na sasa angeweza kuona kila kitu kama kilivyo kwa mara yake ya kwanza.

Kimuujiza Yesu alimponya Kipofu;
Pia aliwalisha watu 5,000 kwa wakati mmoja.

Nifuatisheni mimi: "Ni Mungu pekee awezaye kutenda miujiza."
"Yesu ni Mungu!"

Siku ya Tatu

Yesu anawalisha watu 5,000

Marko 6:34-44

- **Yesu alikuwa anafundisha** kundi kubwa la watu. (Mstari. 34)
- Hatimae **mda ulikuwa umeenda,** Ndipo wanafunzi wake **wakamwambia Yesu Awaruhusu watu waondoke** ili waweze kujipatia chakula katika mji ulio jirani. (Mstari 35-36)
- Yesu akawaambia, **"Wapeni nyinyi chakula."** (Mstari 37a)
- **Wanafunzi walikwazika kwa kile alichosema Yesu** kwa sababu hawakuwa na kiasi cha pesa cha kutosheleza kuwalisha watu wengi kiasi kile. (Mstari. 37b)
- Yesu aliwauliza **ni mikate mingapi waliyokuwa nayo.** (Mstari . 38a)
- TWaliweza kupata tu **Vipande vitano vya mkate na samaki wawili.** (Mstari. 38b)
- Yesu alivichukua vile vipande vya mkate na samaki, akaangalia juu, **na akashukuru.** Mstari. 41a)
- Baada ya kuvimega vile vipande vya mkate, Yesu aliwapa wanafunzi wake Chakula, **na wakawagawia watu.** (Mstari. 41b)
- **Kila mmoja alikuwa na kutosheka!** (Mstari . 42)
- Baada ya kila mmoja kumaliza kula, vilisalia **vikapu kumi na viwili vya mikate na samaki.** (Mstari . 43)
- **ULIZA:** Je Unadhani ni watu wangapi **aliowalisha Yesu** siku ile? (5,000)

Yesu kimuujiza aliwalisha watu 5,000;
Pia alituliza dhoruba.

Sema pamoja nami: "Ni Mungu pekee awezaye kutenda miujiza."
"Yesu ni Mungu!"

Siku ya Tatu

Yesu anatuliza Dhoruba

Marko 4:35-41

- Siku moja jioni, Yesu na wanafunzi wake **waliweka Tanga ili kuvuka ng'ambo** ya bahari ya Galilaya. (Mstari. 36a)

- Walipokuwa juu ya maji, **walikabiliana na dhoruba kali.** (Mstari . 37a)

- **Mawimbi makubwa yaliwapiga kwa ubavuni** mwa boti, na **ilikaribia kuzama**. (Mstari . 37b) **Vitendo:** Tengeneza mawimbi kwa kutumia mikono yako—Juu na chini kama mwendo wa tiara.

- **Yesu alikuwa amejilaza** sehemu ya mbele ya Boti. (Mstari . 38a) **Vitendo:** Kila mmoja na ajifanye kama mwenye usingizi.

- **Wanafunzi walimwamsha Yesu** na wakamwambia, **" Mwalimu, Si kitu kwako kwamba tunaangamia?"** (Mstari 38b)

- "Ndipo aliamka na **kuukemea Upepo [Aliamuru upepo usimame],** na akaiambia Bahari, **" Tulia!**'" (Mstari 39a)

- **Upepo ulitulia mara,** na **mawimbi yakanyamanza kimya.** (Mstari 39b) **Vitendo:** Tengeneza mawimbi kwa kutumia mikono yako mwenyewe, kasha sitisha na kutulia kabisa.

- Yesu aliwauliza wanafunzi **Kwa nini walikuwa na hofu.** (Mstari . 40)

- Hakika waliogopa, na wakajiuliza, " Ni nani huyu, **hata upepo na bahari vinamtii!**'" (Mstari. 41)

- Yesu aliwaonyesha wanafunzi wake kwa mara nyingine kuwa **Yeye ni Mungu kweli** na **anayo mamlaka juu ya kila kitu,** hata juu ya Upepo na bahari.

Yesu alifanya miujiza mingi katika kipindi cha kuishi kwake Duniani,
Na bado anafanya miujiza hata leo.

Sema pamoja nami: "Ni Mungu pekee awezaye kutenda miujiza"
"Yesu ni Mungu!"


Kutengwa na Mungu
Mungu
Dhambi
kufanywa Haki na Mungu
Mungu
Yesu
Dhambi
Siku ya Tatu

Kwa nini Yesu alikuja Ulimwenguni?

Yesu alitenda miujiza mingi, kudhihirisha kuwa ni Mwana wa Mungu. Muujiza mkubwa ni zawadi yako ya Uzima wa milele.

Dhambi zilitutenga wewe na mimi kwa Mungu

Warumi 6:23 ikatika Biblia inasema " Kwa maana **mshahara wa dhambi ni mauti,** bali karama ya Mungu ni Uzima wa Milele katika Kristo Bwana wetu."

Dhambi ni jambo lolote unalolifikiria, utendalo au kutotenda lisilompendeza Mungu.

Ni zipi baadhi ya dhambi? (Kusema uongo, Kudokoa, Kuiba, kumjeruhi mwengine, kutotii wazazi, kutomjali muhitaji, nk...)

Mungu ni Mtakatifu, au Mwema Mkamilifu, Hivyo hawezi kuikubali dhambi. Dhambi inakutenga **wewe** na Mungu.

Kazi: Elekeza kwenye Ufa uliopo kati yako na Mungu.

Adhabu ya Dhambi ni **mauti.**

Maamuzi

Mungu alimtuma Yesu, Mwana pekee, hapa ulimwenguni, takriban miaka 2,000 iliyopita ili **kubeba adhabu ya dhambi zetu** na kutupatia njia ya kuupata Uzima wa milele. (Yohana 3:16).

Ili kuipokea karama ya Mungu ya Uzima wa Milele, Ni **Iazima Ufanye ABC**:

A—Admit = Kubali kwa Mungu kuwa ulitenda dhambi na mambo maovu. Kumbuka Dhambi ni jambo lolote unalolifikiria,utendalo au kutotenda lisilompendeza Mungu.

B—Believe = Amini Kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako na ya kuwa alifufuka kutoka kwa wafu.

C—Choose = Chagua kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wako. **Bwana** inamaanisha unamfanya yeye kuwa **Boss** wa Maisha Yako.

Kazi: Elekeza Msalaba lilipo jina la Yesu, na washirikishe kuwa Yesu alitengeneza njia ya kutufikisha kwa Mungu kupitia kifo chake msalabani.

Mwaliko wa fufanya chaguo

Tafadhali **Inamisheni vichwa vyenu** na kufumba macho yenu sasa.

Nitaenda kuwaombea, au **kusema na Mungu**. **Kazi:** Omba kwamba watoto wapate mwamko wa kuchukua maamuzi. Usimalizie maombi yako kwa kusema " Amen" kwanza.

Iwapo ungehitaji Yesu **akuokoe kutokana na dhambi zako leo,** Tafadhali inua mkono wako sasa.

Iwapo umeinua mkono wako, **simama sasa na elekea** _____ (Elekeza mahali) ambapo yupo atakaye zungumza na wewe kuhusu kumfanya Yesu kuwa Bwana na Mwokozi.

Kazi: Baada ya kila mtoto kusimama na kuondoka, **malizia maombi yako** kwa kumshukuru Bwana kwa msamaha na maisha ya milele. Kisha malizia na **" Amina"**

Siku ya tatu: Maswali ya Rejea ya Somo

1. Je watu walionyesha mwitikio gani, Yesu aliposema kuwa mtoto hajafa? (Walicheka.)
2. Ni kipi alichofanya Yesu kwa Binti aliyekufa? (Alimrejeshea Uhai.)
3. Ni kipi alichofanya Yesu kwa Yule Kiipofu? (Alimponya.)
4. Mara Yule kipofu alipoona kwa mara ya kwanza baada ya kuponywa, Je! Alisema watu wanafanana na nini? (Miti)
5. Ni watu wangapi aliowalisha Yesu? (5,000)
6. Wanafunzi walipopatwa na hofu juu ya dhoruba, Ni nani waliyemkimbilia ndani ya boti? (Yesu)
7. Alifanya nini Yesu juu ya dhoruba? (Aliiamuru isimame, na ikatii.)
8. Ni kipi kinachotutenga na Mungu? (Dhambi)
9. Ni kipi alichofanya Yesu kwa ajili yako na mimi? (Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu.)
10. Anawezaje mtu kuokoka? (Kila ampokeaye Yesu kama Bwana na Mwokozi wake ataokoka.)

Siku ya Tatu: Msalaba wa Shanga

Vitendea kazi:
Pacha au Kamba, Shanga, na Kijimsalaba. Shanga zitatakiwa kuwa na rangi zifuatazo: bluu, Kijani, Manjano, Nyeupe, Nyekundu na Nyeusi. Vifaa vyote hupatikana Stationary.

Jinsi ya kutengeneza:
Chukua pacha au kamba, na ikate kwa urefu wa Sentimita 45—50. Kunja mara mbili kasha pata sehemu ya katikati ya kamba. Sentimeta mbili baada ya sehemu ya kati, funga mafundo mawili. Penyeza shanga na kijimsalaba kwa upande wa pili wa kamba kwa kufuatisha mfuatano huu: Nyeusi, Nyekundu, Nyeupe, Kijimsalaba, Manjano, Kijani, na Bluu. Baada ya kupenyeza shanga zote, Funga tena mafundo mawili baada ya shanga ya mwisho ili kuzizuia kuteleza na kuchomoka.

UJUMBE:
Cheni hii ni ukumbusho wa kazi aliyoifanya Yesu kwa kulipa gharama ya deni la dhambi zako.

- **Nyeusi** inawakilisha Dhambi zako, zinazokutenga wewe na Mungu.
- **Nyekundu** inasimama badala ya damu ya Yesu iliyomwagika msalabani kwa ajili ya dhambi zako.
- **Nyeupe** Inawakilisha msamaha wa Mungu juu ya dhambi zako iwapo utampokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wa Maisha yako.
- **Msalaba** ni alama ya upendo wa Yesu kwako katika kujidhabihu maisha yake msalabani kwa ajili ya dhambi zako.
- **Manjano** inawakilisha Uzima wa Milele mbinguni unaopokea mara unapoamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu na kuwa alikufa kwa ajili ya dhambi zako na ya kuwa alifufuka siku ya tatu.
- **Kijani** inawakilisha ukuaji kiroho. Unapomkubali Yesu kama Mwokozi wako, unahitajika kumfanya Bwana wa maisha yako na kutii neon lake kila siku.
- **Bluu** Ni kwa ajili ya ubatizo. Kama Yesu alivyo batizwa katika mto Yorodani, unatakiwa kubatizwa kama tendo la utii kwa Ubwana wake. (Ubatizo haukuokoi; ila unafanyika katika kutii amri ya Yesu.)

“Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo maandiko, na kuwa alizikwa, na ya kuwa alifufuka siku ya tatu kama yanenavyo maandiko.”

(1 Korintho 15:3-4)

Siku ya Nne
"KUFA NA KUFUFUKA KWA YESU"

Utangulizi

Yesu alikuja ulimwenguni ili kulipa gharama ya dhambi zetu. Dhambi ilianzia Bustanini Edeni na Adamu na Eva. Ilikamilishwa na Yesu. Yesu alipokuja ulimwenguni, alikuja kwa makusudi ya kurejesha uhusiano wtu na Mungu na kutupa sisi " Zawadi" ya Uzima wa Milele.
Somo la leo litazungumzia mateso na uchungu Yesu aliyopitia kwa ajili yetu. Lakini haiishii hapo! Siku ya tatu baada ya mwili wa Yesu kuzikwa kaburini, Yesu alifufuka kutoka kaburini— Alirejea na kuwa mzima tena! Alitembea, aliongea na kula, na watu wengi walimuona Yesu akiwa hai baada ya kusulubiwa kwake.

Yesu yu Hai! Ufufuo wake kutoka kwa wafu ni ishara tosha kuwa ni Mungu na anao uwezo juu ya mauti. Yesu alisema, " Mimi ni ufufuo na uzima". Yeyote aniaminie mimi, ajapokufa, Ataishi". (Yohana 11:25). Kwa sababu Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, tunaweza kufahamu kwa hakika kuwa, pia nasi, tutafufuliwa kwa ajili ya uzima wa milele siku moja.

Mpango wa Kufundisha Mstari wa Kukariri

Mstari wa Kukariri
"**Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kama yanenavyo maandiko, na kuwa alizikwa, na ya kuwa alifufuka siku ya tatu kama yanenavyo maandiko."** (1 Korintho 15:3-4)

Ufafanuzi wa mstari wa kukariri
- Adhabu ya Dhambi zetu ni Mauti.
- Maandiko (Biblia) yanatueleza kuwa Yesu alikufa nafasi yetu kwa ajili ya dhambi zetu.
- Mwili wa Yesu uliokufa ulizikwa kaburini.
- Biblia inaeleza kuwa Yesu alifufuka na kuwa hai tena baada ya kuwemo kaburini kwa siku tatu.
- Kwa sababu Yesu yu hai, pia tunaweza kuishi milele iwapo tukimwamini.

Siku ya Nne

Yesu anashitakiwa mbele ya Pilato

Viongozi katika siku za Yesu walikuwa wenye wivu naye. Yesu alitenda miujiza mingi na kuonyesha upendo wake usio na masharti kwa watu wa siku zake. Kwa ajili hiyo, mamia ya watu walianza kumfuata. Viongozi wa kiroho walipatwa na wivu kwa sababu watu wengi waliacha kuwasikiliza na kuwatii. Walitengeneza uongo juu ya Yesu na wakamkamata na kumpeleka kwa kiongozi wa Kirumi.

Marko 15:1-5, 12-15

- Alfajiri na mapema, wakuu wa Makuhani na viongozi wengine walikutana na **kuamua Yesu akabidhiwe kwa Pilato,** Gavana wa Kirumi. (Mstari 1)
- Pilato alimuuliza Yesu, **"Je! Wewe ni Mfalme wa Wayahudi?"** (Mstari 2a)
- Yesu akajibu, "**Wewe wasema**." (Mstari 2b)
- **Wakuu wa Makuhani** walikuwepo, na **walimshitaki Yesu** kwa mambo mengi sana. (Mstari . 3)
- **"Je! Unalo la kujitetea?** Tazama mambo mengi wanayoyashuhudia kinyume chako!" Pilato alimwambia Yesu. (Mstari . 4)
- Yesu hakusema Neno, Kisha **Pilato alimshangaa Yesu**. (Mstari . 5)
- Pilato akaongea na Umati, **" Mwataka nimtendeje mtu huyu** mnayemwita Mfalme wa Wayahudi?" (Mstari . 12)
- Umati ukapiga kelele, **"Asulubiwe!"** (Mstari 13) **Fafanua:** " Kusulubisha" maana yake Kumtundika mtu na kugongelea miguu na mikono kwa misumari kwa lengo la kumuua.
- Pilato akawauliza **ni kipi amefanya Yesu kinachostahili kifo.** (Mstari 14a)
- "Wakapiga tena kelele zaidi, **" Asulubiwe"!** (Mstari 14b)
- "Hivyo Pilato, akitaka kuuridhisha umma… **akamtoa Yesu kwao, [baada ya kumpiga kwa kipigo kikali] ili asulubiwe.** " (Mstari 15)

Yesu alishitakiwa bila kosa, kama muuaji alipigwa kabla ya kusulubishwa.

Siku ya nne

Kusulubiwa kwa Yesu

Marko 15:16-32

- Askari **wa kirumi walimvisha Yesu nguo ya zambarau,** kisha walitengeneza **taji la miiba** na kumuwekea kichwani pake. (Mstari 17) **Uliza:** Je! Mliwahi kukanyaga mwiba? Unaumiza sana.

- **Walimdhihaki Yesu** na kumfanyia vitimbi na vituko. Walipiga kelele, **" Huyoo Mfalme wa Wayahudi!**" (Mstari 18)

- "Kisha **walimgonga na kitu kizito kichwani pia walimtemea mate;** na kumpigia magoti kwa kusujudu, kama ishara ya kumwabudu." (Mstari 19)

- Baada ya kumkebei na **kumfanyia vituko na vitimbi** kwa mda, walimvua vazi lake lile la zambarau na **wakamuongoza nje ili kumsulubisha.** (Mstari 20)

- Walimpeleka Yesu mahali paitwapo **Golgotha,** maana yake "**Fuvu la kichwa"** (Mstari 22)

- **Walimsulubisha Yesu.** (Mstari 24a) **Fafanua:** Walimtundika mikono na miguu kwenye Msalaba wa mbao.

- Pia **walisulubishwa wanyang'anyi** waliowekwa kila upande wake Yesu. (Mstari 27)

- "Hata wale waliokuwa wakipita maeneo yale **walimzdhihaki [walipiga kelele kwa kutamka maneno mengi kumuhusu]."** (Mstari 29a)

Yesu alitendewa vibaya na kuumizwa sana alipokuwa akisulubishwa.

Siku ya Nne

Yesu Msalabani — Imekwisha!

Marko 15:33-39; John 19:28-30

- Ilikuwa yapata mchana kati, **giza lilifunika nchi.** (Mstari 15:33) **Uliza:** Je linakuwepo giza nje mnapokula chakula cha mchana? (Waruhusu watoto wajibu). Lilitokea giza mchana kati kama inavyokuwa Usiku aliposulubishwa Yesu.

- Ilikuwa saa tisa alhasiri Yesu alipopaza sauti, **" Mungu wangu, Mungu mbona umeniacha?"** (Mstari 15:34)

- "Baada ya haya, Yesu, Huku akijua kuwa mambo yote yamekamilika… alisema " Imekwisha!'...**Akaikabidhi roho yake.**" (Mstari 19:28a, 30b) **Fafanua:** Yesu alikufa. Haukuwemo tena uhai katika mwili wake. Alikuwa amekufa.

- **Fafanua:** Yesu alitambua kabla ya kufa kwake kwamba alichukua juu yake mwenyewe adhabu ya dhambi zote za Ulimwengu.

- **Pazia** la Hekalu lililowatenganisha Mwanadamu na Mungu **lilipasuka vipande viwili** mara tu Yesu alipokata roho. (Mstari 15:38) **Fafanua:** Hii inamaanisha kuwa hatuhitaji tena kuhani kutuwakilishia maombi yetu kwa Mungu. Sasa tunacho kibali cha kumwendea Mungu moja kwa moja, na tunaweza kumuomba moja kwa moja.

- Akida (Askari wa Kirumi) aliyekuwa amesimama pembeni ya msalaba wa Yesu alipoyaona hayo kwamba Yesu amekata roho, alisema, **" Hakika huyu alikuwa Mwana wa Mungu!"** (Mstari 15:39)

Yesu, Mwana wa Mungu, alikufa msalabani
kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.
Alikufa kwa ajili yako na mimi.

Siku ya Nne

Kufufuka kwa Yesu

Yohana 19:38-42; Marko 15:46; Yohana 20:1-8

- "Baada ya haya, Yusufu wa Arimataya...Alimuomba Pilato amruhusu aweze kuuchukua mwili wa Yesu; na pilato alimpa kibali. Hivyo alikuja na **kuubeba mwili wa Yesu**. Na ni-kodemu pia alikuja." (Mstari 19:38-39a)

- **Waliuchukua mwili wa Yesu** na **kuuviringisha kwenye Sanda yenye manukato** kama ilivyokuwa desturi ya Wayahudi. (Mstari 19:40)

- **Kisha wakaulaza mwili wake kaburini.** (Mstari 19:41-42) **Fafanua:** " Kaburi" Ni aina ya shimo ambamo wafu huzikwa. Kaburi la Yesu lilikuwa kama mwamba uliochongwa.

- **Waliufunga mlango wa kaburi kwa jiwe kubwa.** (Mstari 15:46)

- Alfajiri na mapema siku ya tatu, **Mariamu Magdalena alienda kaburini** na kulikuta **jiwe limeviringishwa mbali.** (Mstari 20:1)

- Akakimbia hadi kwa Simoni Petro na Yohana, wanafunzi waliopendwa, na akawaambia **mtu asiyejulikana ameuchukua mwili wa Yesu** kutoka kaburini. (Mstari 20:2)

- Petro na Yohana **wakakimbia kuelekea kaburini.** (Mstari 20:4) **Uliza:** Ni nani mnadhani alitangulia kufika kaburini? (Yohana, lakini hakuingia moja kwa moja)

- "Ndipo Simoni Petro….**akaingia kaburini;** na kuikuta sanda imetupwa pembeni, na leso aliyofungwa kichwani." (Mstari 20:6-7a)

- Ndipo Yohana **akaingia ndani ya kaburi, na kuona kwamba kaburi lilikuwa wazi,** na **akaamini.** (Mstari 20:8)

Mwili wa yesu haukuwemo tena kaburini.
Unadhani ni nini kilimtokea?


Kutengwa na Mungu
Mungu
Dhambi
kufanywa Haki na Mungu
Mungu
Yesu
Dhambi
Siku ya nne

Kwa nini Yesu alitakiwa kufa?

Kumbuka alipokufa Yesu msalabani, kwamba **alitwaa adhabu ya dhambi zako.**

Dhambi inakutenga wewe na Mimi na Mungu

Warumi 6:23 Katika Biblia tunasoma 'Kwa maana **mshahara wa dhambi ni mauti,** bali karama ya Mungu ni uzima wa Milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."

Dhambi ni jambo lolote unalofikiria, usemalo, utendalo, au usilotenda na lisilompendeza Mungu.

Je1 unaweza kuzitaja baadhi ya dhambi? (Kudanganya, kudokoa, Kuiba, kuwaumiza wengine, kutowatii wazazi, kutokumjali muhitaji, nk…)

Kwa sababu ya dhambi zako, umetengwa na Mungu, na umepotea. **Kazi:** Elekeza kwenye ufa kati yako na Mungu.

Mshahara wa dhambi ni **mauti—Kutengwa na Mungu**.

Maamuzi

Mungu alimtuma Yesu, Mwanae wa pekee, ulimwenguni kama miaka 2,000 iliyopita **ili kulipa adhabu ya dhambi zetu** na kutuonyesha sisi njia ya kupata uzima wa milele (Yohana 3:16)

Ili kukipokea kipawa cha Mungu cha uzima wa Milele, ni **lazima ufanye ABC**:

:
A—Admit = Kubali kwa Mungu kuwa ulitenda dhambi na mambo maovu. Kumbuka Dhambi ni jambo lolote unalolifikiria,utendalo au kutotenda lisilompendeza Mungu.
B—Believe = Amini Kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako na ya kuwa alifufuka kutoka kwa wafu.
C—Choose = Chagua kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wako. Bwana inamaanisha unamfanya yeye kuwa **Boss** wa Maisha Yako.

Kazi: Elekeza Msalaba lilipo jina la Yesu, na washirikishe kuwa Yesu alitengeneza njia ya kutufikisha kwa Mungu kupitia kifo chake msalabani.

Mwaliko wa kufanya chaguo
Tafadhali Inamisheni vichwa vyenu na kufumba macho yenu sasa.
Nitaenda kuwaombea, au kusema na Mungu. **Kazi**: Omba kwamba watoto wapate mwamko wa kuchukua maamuzi. Usimalizie maombi yako kwa kusema " Amen" kwanza.
Iwapo ungehitaji Yesu akuokoe kutokana na dhambi zako leo, Tafadhali inua mkono wako sasa.
Iwapo umeinua mkono **wako, simama sasa na elekea** _____ (Elekeza mahali) ambapo yupo atakaye zungumza na wewe kuhusu kumfanya Yesu kuwa Bwana na Mwokozi.
Kazi: Baada ya kila mtoto kusimama na kutoka nje, Malizia **maombi yako** kwa kumshukuru Bwana kwa msamaha na Uzima wa Milele. Malizia na **"Amen"**

C—Choose to receive Jesus as your Savior and Lord. "Lord"

Siku ya NNe: Maswali ya Rejea ya Somo

1. Je! Ni nani waliompeleka Yesu mbele za pilato? (Viongozi wa Kiyahudi)
2. Pilato alipouliza umati kuwa amtendeje Yesu, Je! Walisemaje? (Msulubishe!")
3. Nini alichokifanya Pilato dhidi ya Yesu kabla hajamkabidhi kwa Umati? (Achapwe viboko)
4. Nini kilitengeneza taji alilowekewa Yesu na Wanajeshi kichwani? (Miiba)
5. Je! Ni kipi alichofanya Yesu kilichosababisha auawe kama mnyang'anyi? (Hajatenda kosa lolote)
6. Nini kilitokea siku tatu baada ya kifo cha Yesu? (Alifufuka kutoka kwa wafu)
7. Yesu alisulubiwa kkatikati ya watu wawili. Je! Watu hao wawili walifanya nini kili-chowasababishia hukumu hiyo ya kifo? (Walikuwa wanyang'anyi)
8. Nini kilichotokea mchana wa siku ya Kusulubiwa kwa Yesu? (Lilitokea Giza).
9. Je! Nini kwa nini Yesu aliuawa? (Kwa ajili ya dhambi zetu)
10. Nini kilitokea siku tatu baada ya kifo cha Yesu? (Alifufuka kutoka kwa wafu)

Siku ya Nne: Sanaa ya Kitabu kisicho na maneno



Vitendea kazi:
Karatasi za Ujenzi (Ngumu) (Nyeusi, Nyekundu, Nyeupe, Manjano, na Kijani), Gundi ya Shule, Mkasi au kikata karatasi

Kitabu kisicho na maneno ni Sanaa nyepesi sana yenye Ujumbe wenye nguvu. Kinatokea kuwa kifaa cha kushirikisha Injili na kumbukumbu kwa mtoto aliye potea au aliyeokoka juu zawadi ya Mungu ya Uzima wa Milele.

Jinsi ya kuiandaa sanaa hiyo:

1. Kwa kutumia kikata karatasi au Mkasi, kata karatasi ya kujengea (Ngumu) katika vipande usawa wa robo. Iwapo unatumia mkasi unaweza kuikunja kila karatasi kwa nusu, kisha ikunje tena kwa nusu ya pili. Tumia mistari inayotokeza kama alama nzuri ya kukatia. (Tazama hapo chini).
2. Baada ya kuvikata vipande vyako katika vipimo vinavyoeleweka, vikunje kwa kati kila kipande. (A)
3. Kifungue kipande cha kijani na kilaze juu ya meza kikiwa kimenyooka na Mkunjo wa kati ukiwa wima. Kisha weka kipande kilichokunjwa cheusi kwenye nusu ya karatasi ya Kijani, Upande wa Kushoto, mkunjo ukiulenga kwenye ule mkunjo wa ile karatasi ya kijani. Tumia Gundi kati ya karatasi ya Kijani na ile Nyeusi. (B)
4. Ile karatasi ya kijani itabaki wazi na ile nyeusi ikiwa imekunjwa, weka ile Nyekundu iliyokunjwa kwenye ile nyeusi, Mkunjo ukiwekwa usawa wa ule wa kijani uliosimama. Weka Gundi kati ya Kati ya karatasi nyeusi na ile ya Nyekundu. (C)
5. Karatasi ya kijani ikizidi kuwa wazi, na Nyeusi na nyekundu zikiwa zimkunjwa, weka karatasi nyeupe iliyokunjwa juu ya ile Nyekundu, Mkunjo ukiwekwa usawa wa ule wa Kijani uliosimama. Weka Gundi kati ya karatasi Nyekundu na ile Nyeupe. (D)
6. Karatasi ya kijani ikizidi kuwa wazi, na Nyeusi, nyekundu na Nyeupe zikiwa zimkunjwa, weka karatasi ya Manjano iliyokunjwa juu ya ile Nyeupe, Mkunjo ukiwekwa usawa wa ule wa Kijani uliosimama. Weka Gundi kati ya karatasi Nyeupe na ile ya Manjano. (E)
7. Kile kipande cha Manjano kikiwa kimekunjwa, weka Gundi kati ya Karatasi ya Manjano na kipande cha pili cha kijani upande wa kulia ili kukikamilisha kitabu.
8. Kurasa zitatakiwa kufunguka ili ionekane rangi moja tu kila mara unapofungua ukurasa. Kinapofungwa, kitabu chako kitaonyesha tu Ganda la kijani kwa mbele na nyuma. (F)

Ujumbe:
Kitabu kisicho na maneno kinao ujumbe wa ajabu sana ndani yake. Katika kukitumia kitabu hiki, unaweza kumsaidia mtu kuielewa Injili ili kwamba aweze kufanya maamuzi binafsi kwa ajili ya Kristo na kupata kuokolewa.

Nyeusi.. Ukurasa mweusi unawakilisha dhambi. Dhambi ni jambo lolote unalofikiri, usemalo, ufanyalo, au usilolifanya lisilompendeza Mungu. (Warumi 6:23)

Nyekundu… Ukurasa mwekundu unawakilisha damu ya Yesu, aliyekufa msalabani kwa ajili yetu. (1 Wakorintho 15:3-4)

Nyeupe… Ukurasa Mweupe unawakilisha Msamaha. Tunaapoamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu , Tunapata msamaha wa dhambi zetu. (Yohana 1:12)

Yellow.. The yellow page stands for eternal life. When we accept Christ as our Savior and Lord, we will spend eternity with Him in Heaven one day. (John 3:16)









“Bali wote wali-ompokea aliwa uwe-zo wa kufanyika wa-toto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.”

(Yohana 1:12)

SIKU YA TANO
"PAUL: MAISHA YA KIKRISTO"

Utangulizi

Paul alikuwa kiongozi muhimu wa kiyahudi katika siku zake. Pia alikuwa mtu wa dini sana. Alimpenda Mungu lakini hakujua kwa hakika aliyekuwa Mwana wa Mungu hadi alipokutana na Yesu njiani kuelekea Dameski. Tutajifunza kumuhusu Paul katika somo letu la leo.

Mpango wa kufundisha mstari wa Kukariri

Mstari wa kukariri

""Bali wote **waliompokea** aliwa uwezo wa kufanyika **watoto wa Mungu**, ndio wale **waliamin-io jina lake."** (Yohana 1:12)

Ufafanuzi wa Mstari wa Kukariri

- Watu wakati mwingine wanaamini kuwa zipo njia nyingi za kwenda mbinguni, lakini ipo njia moja tu—Yesu Kristo.
- Lazima uchague kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wako.
- Lazima uamini kuwa ni mwana wa Mungu.
- Unapompokea Yesu, Unafanyika Mwana wa Mungu.

Rejea ya siku zilizopita

- Kumbuka, Mungu aliumba kila kitu.
- Kwa ajili ya Mtu mmoja (Adamu), dhambi iliingia ulimwenguni mwote.
- Wote tulihesabika wenye dhambi kwa ajili ya Adamu.
- Mungu alimtuma Yesu kubeba ghazabu ya dhambi zetu alipokufa msalabani.
- Tunaweza kuokolewa kwa kumwamini Yesu pekee kama Mwokozi wetu na kumfanye yeye kuwa Bwana na Boss wetu.

Siku ya Tano

Muhtasari wa Somo

Kubadilika kwa Paul

Acts 9:1-20

- "Lakini Sauli, akizidi **kutisha na kuwaza kuwaua** wanafunzi wa Bwana [akiongea maba-ya kinyume na wakristo]." (Mstari 1) **Fafanua:** Jina la asili la Paul lilikuwa Sauli kabla hajafanyika Mkristo.

- Hata alipokuwa akisafiri, ikawa **anakaribia Dameski**; ghafula ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni. (Mstari 3).

- "Kisha alianguka chini, na akasikia sauti ikimwambia, " Sauli, Sauli, **Mbona waniudhi**?" (Mstari 4) **Fafanua:** "Kuudhi" maana yake kumkataa au kuwa kwazo kwa mtu Fulani kutokana na imani yake. Uli alikuwa kwazo kwa Wakristo, Lakini Yesu alilichuka kama muhusika binafsi.

- "**Wewe ni nani Bwana?**" Aliuliza Sauli (Mstari 5a)

- "Ndipo Bwana akasema, '**Mimi ndimi Yesu**, Unayeniudhi" (Mstari 5b)

- Yesu alimwambia Sauli **Nenda katika mji** Na nitakuelekeza yakupasayo kutenda. (Mstari 6)

- Sauli alipoinuka, hakuweza kuona tena. **Alikuwa kipofu.** (Mstari 8) Alioongozana nao **walimshika mkono hadi mjini.**

- Mwanafunzi mmoja wa Yesu aliyeitwa **Anania aliishi Dameski** (Mstari wa 10a)

- **Yesu akasema na Anania** katika ndoto na kumwambia ni wapi angempata Sauli ili aweze **kumrejeshea Sauli kuona**. (Mstari 10-12)

- **Anania alipatwa na hofu ya Sauli** sababu alikuwa anaelekea Dameski kuwafunga wa-fuasi wote wa Yesu. (Mstari 13-14)

- "Lakini Bwana Akamwambia [Anania], 'Nenda, **maana ni chombo change kiteule** ili kulibeba Jina langu mbele ya mataifa, wafalme na Wana wa Israeli.'" (Mstari 15)

- Anania akaenda **hadi nyumba alimokuwemo Sauli** na akamuwekea Sauli mkono. (Mstari 17)

- "Akasema, Ndugu Sauli, **Bwana Yesu,** aliyekutokea njiani ulipokuwa ukielekea huku, **amenituma** kwamba upate kuona na kujazwa na Roho Mtakatifu.'" (Mstari 17)

- Ghafla, **Sauli alipata kuona tena.** (Mstari 18a)

- **Uliza:** Je! Unadhani ni nini Paul alifanya baadae? Je angeweza kumfuata Yesu?

Yesu anaweza kubadilisha maisha,
Hata wale wanaoonekana wapinzani sana kwake.

Siku ya Tano

Mahubiri ya Paul

Matendo 13:1-5; 14:1, 21-22

- Katika kanisa la Antiokia, walikuwepo **walimu, Viongozi, na manabii** wa Kikristo na Sauli [Paul] akafanyika mmoja wao. (Mstari 13:1)

- "walipokuwa **wakihudumu kwa ajili ya Kristo na kufunga,** Roho Mtakatifu ailiwaambia, " Sasa **Nitengeeni Barnaba na Paul** kwa ajili ya kazi niliyowaitia.'" (Mstari 13:2)

- **Walifunga, Waliomba, na wakaweka mikono juu ya** Barnaba na Paul. (Mstari 13:3a)

- Kisha **Wakawatuma** (Mstari 13:3)

- Wakitumwa na Roho Mtakatifu, Barnabas na Sauli [Paul] **waliteremkia hadi Seleukia,** na wakasafiri **baharini hata Kipro**. (Mstari 13:4)

- Na walipokuwa katika Salami **walifundisha kumuhusu Yesu** katika masinagogi ya Wayahudi (Mstari 13:5a)

- **Yohana aliongozana nao** kama msaidizi (Mstari 13:5b)

- "Sasa ilitokea huko IKONIO kwamba waliongozana kwenye Sinagogi la Wayahudi, na wakasema na **kundi kubwa la watu wakichanganyika Wayahudi, na Wayunani waka-mini**." (Mstari 14:1)

- Ndipo baadae **walirudi kwenye makanisa** waliyoyaanzisha **ili kufundisha na kuwatia moyo waamini** wabaki waaminifu kwa Bwana. (Mistari 14:21b-22a)

- Paul aliwafikia watu wengi sana na Ujumbe wa Yesu Kristo, na **Alieneza huduma yake kupitia Nyaraka zake** kwa makanisa tofauti aliyoyaanzisha.

Yesu alimtumia Paul kuieneza Injili,
Na barua zake (ndani ya Biblia) zinaendelea kutufundisha hadi leo.

siku ya tano

Nyaraka za Paul kwa Kanisa

Paul aliandika vitabu vingi vya Agano Jipya ndani ya Biblia. Vitabu hivi vinaitwa Nyaraka. Makusudi ya Vitabu vyake, au Nyaraka, ilikuwa nikuendelea kushirikisha mafundisho ju Kristo kati ya waamini wengi wapya aliokutana nao katika Asia.

Paul aliandika Nyaraka hizi zaidi ya miaka 2,000 iliyopita, na mafundisho yake juu ya Yesu yamekuwa na manufaa kwa mamilioni ya watu ulimwenguni mwote wakati uliopita hata sasa.

Paul Aliandika Nyaraka zifuatazo ndani ya Biblia, ambazo kwa asili zilielekezwa kwa makanisa ya kwanza ya Kikristo.

- Warumi
- 1 & 2 Wakorintho
- Wagalatia
- Waefeso
- Wafilipi
- Wakilosai
- 1 & 2 Wathesaloniki
- 1 & 2 Timotheo
- Tito
- Filemoni

Acha tuone jinsi ya kuvipitia baadhi ya vitabu hivi ndani ya Biblia.


Talk With God
Tell Others
Jesus is LORD
Gifts & Ministry
Life of Obedience
Read The Bible

Ni zipi hatua zinazofuatia baada ya kumpokea Kristo?

Unaweza kujifunza kuishi kwa ajili ya Yesu ukiutumia msalaba. **Kazi:** Elekeza picha ya msalaba. Msalaba unatupa hatua rahisi za kumfuata Yesu.

Luka 9:23 says, “Kisha akawaambia, Mtu akitaka kunifuata, **na ajikane mwenyewe,** na **ajitwike msalaba wake kila siku,** na **anifuate**.’”

Msalaba unatufundisha kuishi kwa ajili ya Yesu kila siku.

1. **Yesu ni Bwana—**Mfanye Yesu kuwa Boss wa maisha yako kila siku.
2. **Waambie na wengine**— waambie marafiki zako na wanafamilia kumuhusu Yesu. Fafanua ABCs kwao ili waweze kujua ni jinsi gani ya kumpokea Yesu kama Mwokozi wao.
3. **Zungumza na Mungu**—Omba kila siku. Unaweza kuzungumza na Mungu muda wowote, mahali popote.
4. **Vipawa na Huduma**—Mtumikie Mungu kila siku. Tumia karama alizokupa ili kuwatanguliza wengine.
5. **Soma Biblia**—Biblia ni kitabu cha Maelekezo ya Mungu kwa ajili ya maisha yako. Kwa njia ya kujisomea Neno la Mungu, utagundua ni jinsi gani Yesu anataka uyaishi maisha yako. Pia ni barua ya upendo itokayo kwake kuja kwako.
6. **Maisha ya Utii**—Fanya kile Yesu anachosema kila siku.

Hizi ni hatua kwa wale wanamjua Yesu kama Bwana na Mwokozi. Huwezi kuianza safari hadi umepata mahali pa kuanzia ambapo ni Yesu. Yesu ni zawadi kwa sababu anatupatia zawadi ya Uzima wa milele kwa kila mmoja anayemwamini.

Acha turejee tena mara moja
Unawezaje kuianza safari yako pamoja na Yesu Leo.


Kutengwa na Mungu
Mungu
Dhambi
kufanywa Haki na Mungu
Mungu
Yesu
Dhambi
Siku ya Tano

Kwa nini Yesu alikuja Ulimwenguni?

Kumbuka, Yesu alikuja ulimwenguni sababu **Dhambi zetu zilitutenga na Mungu.**

Paul alikuwa kiongoza wa dini katika siku zake, lakini alikuwa amepotea sababu hakumjua Kristo. Kwenda kanisani au kutenda mema kwa ajili ya Mungu hayakufanyi uokoke. Unalo tatizo—DHAMBI!

DHAMBI: Zinakutenga wewe na Mimi na Mungu

Warumi 6:23 katika Biblia inasema, " **kwa maana mshahara wa Dhambi ni mauti,** bali karama ya Mungu ni Uzima wa Milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."

Dhambi ni jambo lolote unalolifikiria, usemalo, utendalo, au kutotenda lisilompendeza Mungu.

Je unaweza kutaja baadhi ya Dhambi? (Kudanganya, Kudokoa, Kuiba, Kumjeruhi mwengine, kutoheshimu wazazi, kutomjali muhitaji nk…)

Kwa sababu ya Dhambi zako, umetengwa na Mungu, na umepotea. **Kazi:** Elekeza kwenye Ufa kati yako na Mungu.

Mshahara wa Dhambi ni **Mauti—Kutengwa na Mungu**.

Kwa sababu ya dhambi zako, **umetengwa na Mungu,** kama jinsi hii picha inavyoonyesha. **Kazi:** Elekeza kwa Ulimwengu, ambao unamuwakilisha kila mmoja wetu.

Mungu alilitimiza ahadi yake kwa kumtuma **Mwokozi aje kutuokoa kutokana na Dhambi zetu. Kazi:** Elekeza kwenye Msalaba wa Rangi ya Udongo Usemao " Yesu."

Maamuzi

Mungu alimtuma Yesu, Mwanae mmoja na wapekee hapa Duniani takriban miaka 2000 iliyopita ili **kuichukua adhabu ya dhambi zetu** na kutupa njia ya kuupata Uzima wa Milele. (Yohana 3:16)

Ili kukipokea kipawa cha Mungu cha uzima wa Milele, ni **lazima ufanye ABC:**
:
A—Admit = Kubali kwa Mungu kuwa ulitenda dhambi na mambo maovu. Kumbuka Dhambi ni jambo lolote unalolifikiria,utendalo au kutotenda lisilompendeza Mungu.
B—Believe = Amini Kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako na ya kuwa alifufuka kutoka kwa wafu.
C—Choose = Chagua kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wako. Bwana inamaanisha unamfanya yeye kuwa **Boss** wa Maisha Yako.

Kazi: Elekeza Msalaba lilipo jina la Yesu, na washirikishe kuwa Yesu alitengeneza njia ya kutufikisha kwa Mungu kupitia kifo chake msalabani.

Mwaliko wa kufanya chaguo
Tafadhali Inamisheni vichwa vyenu na kufumba macho yenu sasa.
Nitaenda kuwaombea, au kusema na Mungu. **Kazi**: Omba kwamba watoto wapate mwamko wa kuchukua maamuzi. Usimalizie maombi yako kwa kusema " Amen" kwanza.
Iwapo ungehitaji Yesu akuokoe kutokana na dhambi zako leo, Tafadhali inua mkono wako sasa.
Iwapo umeinua mkono wako, **simama sasa na elekea** _____ (Elekeza mahali) ambapo yupo atakaye zungumza na wewe kuhusu kumfanya Yesu kuwa Bwana na Mwokozi.
Kazi: Baada ya kila mtoto kusimama na kutoka nje, Malizia **maombi yako** kwa kumshukuru Bwana kwa msamaha na Uzima wa Milele. Malizia na **"Amen"**
rnal life, **you must ABC**:
A—Admit to God that you have sinned and done wrong

Siku ya Tano: Maswali ya Rejea ya Somo

1. Ni Nani aliye msimamisha Paul njiani kuelekea Dameski? (Yesu)
2. Nini kilichomtokea Paul machoni? (Alipata Upofu.)
3. Nini kilichomtokea Paul baada ya kuombewa na Anania? (Aliweza kuona tena.)
4. Nini alichokifanya Paul baada ya kumtambua Yesu ni Nani (Alianza kumwambia kila mtu juu ya Yesu ns kile alichokifanya juu ya dhambi zao.)
5. Ni kwa njia gani Paul aliongea na watu alio waongoza kwa Yesu? (Aliwaandikia Barua.)
6. Ni nani aliye andika vitabu vingi vya Agano jipya? (Paul)
7. Bibli ni nini? (Neno la Mungu)
8. Biblia inahusu nini? (Mungu na Upendo wake kwako)
9. Kwa nini tunahitaji kusoma Biblia? (Inatueleza ni jinsi gani tuishi kwa kumpendeza Mungu)
10. Kwa nini tunahitaji kuwaambia marafiki habari za Yesu? (Bila yeye wamepotea.)

Sanaa ya Msalaba

Vitendea Kazi:
Nakala za Msalaba, kalamu ya Wino, Kalamu za risasi, Kalamu za risasi za rangi, Maka peni.

Jinsi ya Kutengeneza:
Kwa kutumia karatasi ngumu, Tengeneza nakala nyingi za msalaba kwenye ukurasa wa 74, kisha ikate kate. Mpatie kila mtoto Mtoto msalaba atakao chora na kupaka rangi. Waonyeshe msalaba uliokamilika na na lebo zilizoandikwa tayari kuwa: Yesu ni Bwana, Sema na Mungu, Soma Biblia, Waambie na wengine, na Watumikie na wengine. Wapatie kalamu za wino, Kalamu za Risasi, Kalamu za risasi za Rangi, na Maka peni ili watumie kuwekea alama na kupakaa misalaba yao.

Ujumbe:
- Sanaa ya leo inakusaidia kukumbuka kwamba kuishi kwa ajili ya Yesu ni jambo utendalo kila leo maishani mwako.
- Somo la Biblia la Juma hili linaweza kuwa kama kukumbushia, lakini Yesu ameahidi kuwa pamoja nawe maisha yako yote yaliyo salia.
- Biblia inasema, " Sitawaacha wala sitawapungukia." (Waebrania 13:5)
- Alama ya Msalaba itakukumbusha jinsi ya kuishi kwa ajili ya Yesu kila siku.
- Unaweza kuutumia msalaba kama alama, ubandike kwenye kioo sehemu ya kuogea au mahali pengine popote utakapouona kwa urahisi, au ufunge kipande cha kamba kisha uning'inize.
- Kumbuka, Unapomfanya Yesu kuwa Bwana wa Maisha yako (Sehemu ya kati), Utatamani kuishi maishi ya unyenyekevu kwake katika kuzungumza naye kila siku (Sehemu ya juu), Kuisoma Biblia yako kila siku (Sehemu ya Chini), Kuwaambia na wengine habari za Yesu (Sehemu ya kushoto), na kuwatumikia wengine kwa jina lake (Sehemu ya Kulia).













Siku ya Tano

Ninawezaje kupata ninachokitafuta ndani ya Biblia?

Biblia imetokea kuwa kitabu kikubwa, na ndivyo kilivyo. Hilo lisikutishe katika kubaini **Uhalisia wa Mungu** na kugundua mengu kuhusu **mpango wake wa ajabu kwa ajili ya maisha yako.** 2Timotheo 2:15 inasema, " Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, Mtendakazi asiye na sababu ya kutahayari, Ukilitumia kwa halali Neno la kweli." Biblia ni Neno la Mungu. Mungu aliwavuvia watu maiaka iliyopita ili waandike maneno ya Biblia kwa ajili yetu ili tuweze kujua jinsi ya kuyaishi maisha yetu.

Kutafuta mistari ya Biblia
Biblia ni kitabu kipana chenye vijitabu vidogo vidogo vingi ndani yake. Fungua kurasa za mbele za Biblia yako mahali pa **Yaliyomo,** kisha tafuta kitabu unachokihitaji (Mathayo, Marko, Luka, nk...). Kwa mble, Angalia namba ya ukurasa.

Yaliyomo

AGANO JIPYA

Mathayo.....1
Marko.....46
Luka.....83
Yohana.....147
Matendo.....179
Warumi.....201
I Korintho.....222
II Korintho.....226
Wagalatia.....254
Waefeso.....278
Philippians.....307

Unapoupata ukurasa wa Kitabu unachokihitaji, funua kwenye ukurasa huo. Utakuwa umefika kwenye ukurasa wa Sura ya kwanza ya kitabu hicho. Biblia imegawanyika katika **vitabu, Sura, na mistari.** Iwapo mtu atasema, " Fungua Yohana 1:12," Wanamaanisha Ufungue Kitabu cha Yohana, Sura ya 1, na mstari 12. Tazama mfano ufuatao:



Inua Biblia kisha tamka,
"Biblia ni Neno la Mungu.
Every word in it is true and can be trusted."



L.I.T. Ministries
412 Mercedes, Suite F
Benbrook, Texas 76126